**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OR – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**
**SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-LUMYOZI**

Simu : +255 784241011
+255 652688932
+255 780835747

S. L.P. 33
Kibiti -Pwani

**KUMB.NA. ED/DSL/J.1/25**
…………………………………….
…………………………………….
…………………………………….

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO …….** katika shule ya Sekondari Dr.Samia-Lumyozi katika Tahasusi ya…EGM, HGK /HKL Tunampongeza kwa mafanikio hayo.
Shule itafunguliwa tarehe ………... na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe
………….
Shule ya Sekondari Dr.samia-lumyozi ipo katika **Mkoa** wa **Pwani Wilaya ya Kibiti kata ya Kibiti** umbali wa kilomita 116, Kutoka Dar-es-Salaam.

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-LUMYOZI**
Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara) washuke Kibiti stand.Kuna umbali wa kilomita tano kutoka stand ya Kibiti mpaka shule ilipo, hivyo usafiri wa kutoka Kibiti stand hadi shuleni ni wa pikipiki au bajaji.

Kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike DAR ES SALAAM stand ya mabasi MBAGALA RANGI TATU hapo watapanda Magari yanayoelekea Kibiti, Rufiji, au mabasi yanayoelekea mikoa ya kusini pia nao watashuka kibiti stand.
Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A - G**

A. Maelezo Maalumu Ya Kujiunga Na Shule
B. Michango mbalimbali ya shule.
C. Sheria, Kanuni na taratibu za shule
D. Fomu ya ya Afya (Mwanafunzi apimwe na ijazwe na Daktari aliyemhudumia)
E. Ahadi/Kiapo cha mwanafunzi.

F. Vitabu
G. Vifaa Vya usafi.

Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote. Ni vyema Mzazi/Mlezi umtimizie mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima. Kama kuna changamoto au maswali yeyote unaweza kupiga simu kwa namba zilizoainishwa hapo juu.Karibu sana shule ya sekondari Dr.Samia-lumyozi.

## A. MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE

1.
**SARE KWA WAVULANA**
**a/ Suruali mbili za rangi ya kijivu (steel grey) za darasani ( inapatikana shuleni)**
**b/ Suruali mbili za dark blue kitambaa kizito za kushindia (shamba dress)**
**c/ Shati nyeupe mbili za mikono mirefu**
**d/** T-shirt mbili rangi ya Gold zenye kola zenye nembo ya shule (zitapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/=(@ kwa anayehitaji )
**e/** Tai mbili ndefu za rangi ya kijivu (steel grey)

**MAHITAJI MENGINE:**

a. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (Jozi 2)
b. Soksi ndefu (free size) jozi 2 au zaidi nyeupe.
c. Viatu vya michezo.
d. Kandambili kwa ajili ya kuogea tun a viatu vya wazi (sendoz)zisizo na visigino virefu
e. Sweta moja la **Dark Bluu** lenye shepu ya V.
f. Kila mwanafunzi lazima aje na Tracksuti ya blue bahari ambayo ataivaa siku za mwisho wa wiki.
g. Kila mwanafunzi lazima afunguliwe akaunti Benki NMB au CRDB kwa ajili ya kuhifadhia fedha zake za matumizi. Mwanafunzi atakaguliwa kadi ya benki wakati wa kuripoti shuleni
h. Wakati wa kujisomea usiku mwanafunzi atavaa shamba dress na iwe pana isiyobana pia atavaa sox nyeusi ndefu free size
i. Kila mwanafunzi aje na T shirt ya rangi ya bluu yenye kola maarufu kama form six isiyo na maandishi wala urembo
j. Kila mwanafunzi aje na nguo za kulalia nyeupe (Pajama)
k. Sare za shule zitavaliwa na mwanafunzi kulingana na ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani,Pia mwanafunzi harusiwi kuja na urembo wa aina yeyote ,kunyoa kipara au kufuga nywele ,kutumia madawa ya nywele na ya kujichubua, Pi Mwanafunzi hatakiwi kuvaa pete,
bangili ,hirizi au heleni. Mwanafunzi anaruhusiwa kuweka alama za majina katika nguo zake ili kuepuka usumbufu wa kupoteza au kubadilishana nguo.
l. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kadi ya Bima ya Afya

2. <u>**MAHITAJI YA BWENI**</u>

i. Godoro la nchi $2\frac{1}{2}$ Kwa 6
ii Shuka rangi ya bluu bahari Jozi mbili
iii Mto na foronya 2 za pink na Taulo
iv Nguo za ndani, Vest nyeupe zisizo na urembo na mashine za kunyolea nywele.
v . Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko lita 20
vi . Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili

vii . Vyombo vya chakula, Sahani, Bakuli,Kikombe, Kijiko, Chupa ya chai anaweza kuja na **HOT POT** 1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya.

viii .Chandarua futi 3x6. Ya pembe nne. Pia kila mwanafunzi lazima aje na dawa ya mbu ya kujipaka kwa ajili ya kujilinda na mbu wanaosambaza Malaria.

3. **MAHITAJI YA TAALUMA**

a) **Rimu 2 kwa mwaka (size A4 ) aina ya GSM**

b) Madaftari 06 (Counter Book), Kalamu/Penseli za kutosha

c) Faili 2 kwa ajili ya kuhifazia mitihani na kumbukumbu zingine ‘**’Folder file’’ NB: Baadhi ya mahitaji yanapatikana duka la shule kama Godoro, chandarua, ndoo, Rimu,vifaa vya usafi,vyombo vya chakula n.k**

## B. MICHANGO MBALIMBALI:
## JEDWALI LA MICHANGO MBALI MBALI

| S/N | MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Kuendesha shule | 65,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| 5 | Tahadhari | 5,000/= |
| 6 | Nembo | 5,000/= |
| **7** | **JUMLA KUU** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye Akaunti Namba **21310049005 NMB**
Jina la Akaunti ya shule ni **DR.SAMIA-LUMYOZI SECONDARY SCHOOL CAP Utapata** huduma katika tawi lolote la Benki ya NMB Tanzania.**Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi.**
Mwanafunzi aje na **PAY INSLIP** ya benki wakati wa kuripoti shuleni, **kamwe hatutapokea pesa mkononi.**

## C: SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya **HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA** kwa ujumla

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri Kwa heshima na tabia, kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi
   (a) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.
   (b) Kufuga kucha na nywele
   (c) Kufuga ndevu
   (d) Kunyoa kipara
   (e) Kumpiga mwenzake
   (f) Kutukana
   (g) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (h) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi Kwa kuwa Shule hii ni ya **Serikali**.
   (i) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu

(j) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
(k) Kuvaa suruali chini ya kiuno
(l) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model

4. Mwanafunzi atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu Kwa wengine anapokuwa Darasani, Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prepo) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk
7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:-
   A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya darasa na Mabaraza ya shuleE.Siku ya Jumamosi maandalio ya masomo yataanza saa 4 asubuhi hadi saa 7 mchana
8. Ni LAZIMA mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na KITAMBULISHO kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:-

9. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, anapaswa kuwa na kibali (Pass) cha maandishi.(Kilichotolewa na Mkuu wa shule)

11`. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia **electrical heater** au jiko la aina yoyote

12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.
13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi Kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule ya sekondari Dr.Samia-Lumyozi muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati au T shirt yake. **Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.**
15. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu **kama laini, Charger earphone, Ipadi nk.**
16. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.
17. **MAENEO YASIYORUHUSIWA**:

Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu

- Ofisi za shule
- Chumba cha wafanyakazi
- Maabara
- Jikoni
- Nyumba za wafanyakazi
- Nyumba za ibada

**Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea maeneo yafuatayo**

- Vilabu vya pombe ``````
- Majumba ya starehe
- Majumba ya kufikia wageni

18. **BWENINI**
    - Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake

- Mwanafunzi lazima awepo bwenini kwenye ukaguzi kila siku ya jumatano asubuhi.
- Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote bwenini wakati wote. • Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali aliyokabidhiwa bwenini
- Ni marufuku kupeleka viti ,meza na chakula Bwenini.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti.
3. Ulevi wa aina yoyote.
4. Utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi,Kubeli nk.
5. Uvutaji wa sigara au Bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kuoa au kuolewa
8. Kuharibu Kwa makusudi Mali ya umma.
9. Kupigana au kumpiga mwingine.
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote
13. Kutoa lugha ya matusi
14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
15. Kutohudhuria vipindi
16. Ubakaji.
17. Kuwa na simu ya mkononi au kumiliki line ya simu..

## MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- Medical examination fomu ambayo itajazwa na mganga wa Hospitali ya Serikali mara tu atakapowasili shuleni na kuikabidhi.
- Fomu ya Melezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai
- Fomu ya mzazi kukiri kukubalina na sheria ,kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule

RAMADHANI SEIF MWEMA
MKUU WA SHULE




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OR – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**

**SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-LUMYOZI**

S.L.P 33
KIBITI-.PWANI

**MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi…………………….…………………… …………
2. Kidato …………………mchepuo…….………..mwaka……………
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………
4. Kabila la mwanafunzi………………………………………………..
5. Uraia wa mwanafunzi……………………………………………..
6. Tarehe ya kujiunga na shule ya sekondari ya Dr.Samia-Lumyozi………………………………..
7. Shule aliyotoka ya sekondari (kidato cha tano)…………………………………………………..
8. Masomo.utakayokuja..kusoma………………………………………………………………
9. Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu…………………………………………………………
10. Je unarudia kidato?.......……….
    kwa nini?.......................................................................................................................................
11. Dini ya mwanafunzi…………………….……Dhehebu……………………………………………
12. Anwani ya kudumu ya mwanafunzi
    S.L.P………………………………………………………….

Wilaya……………………………………………….Mkoa………………………………
Tarafa………………………………………………Kata…………………………………
Kijiji/Mtaa…………………………………………………Namba ya nyumba……………

Simu ya nyumbani…………………………………………………………
Simu ya ofisini…………………………………………………………………

**BABA**

13. Jina la Baba……………………………………………………………………………….
14. Je,yu hai ?…………………………………………………………………………………………
15. Kabila la baba……………………………………………………………………………….…
16.Anwani_yake..ya..sasa…………………………………………………………………….……
16. Kazi yake…………………………………………………………………….………
17. Mwajiri wake……………………………………………………………………………………
18. Dini ya baba …………………………..dhehebu……………………………………

19. Je,baba na mama wanaishi pamoja?.......................................................................................

20. Simu ya baba……………………………………Ya kazini……………………………………

**MAMA**

21. Jina la mama………………………………………………………………………………
22. Je,yu kohai?........................................................................................................................
23. Kabila la mama……………………………………………………………………………….
24. Mwajiri wake ………………………………………………………………………………...
25. Anwani yake ya sasa……………………………………………………………………………………….
26. Dini ya mama…………………………………………Dhehebu…………………………………………….
27. Kazi yake ………………………………………
28. mwajili wake…………………………………
29. Simu ya nyumbani……………………… ….Ya ofisini………………………………………..

**MLEZI**

30. Jina la mlezi…………………………………………………………………………………
31. Kabila la mlezi……………………………………………………………………………………………….
32. Uhusiano na mwanafunzi ukoje?...........................................................................................................................
33. Anwani ya sasa……………………………………………………………………………………………
34. Kazi yake……………………………………………………………………………………………
35.Mwajiri. wake………………………………………………………………………………..
35. Dini ya mlezi……………………………………Dhehebu……………………………………
36. Simu ya nyumbani………………………………………..Yakazini…………………………..

**NDUGU WENGINE**

| JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**KIBITI DISTRICT COUNCIL**

**DR.SAMIA-LUMYOZI SECONDARY SCHOOL**

Simu : +255 784241011

+255 652688932
+255 780835747

S. L.P. 33
Kibiti -Pwani

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART 'A'**
TO THE MEDICAL OFFICER
………………………………...
………………………………...

FROM………………………
………………………………
………………………………

Mr./Miss……………………………………………………………………………(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I (a) Eyesight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) Venereal Diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

II Neuroses

III Other serious diseases

Date……………………………………… Signature……………………………………

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…………………… (e) Venereal Diseases………………… (b) Hearing……………………. (f) Leprosy……………………………... (c) Speech …………………….

(d) Limbs…………………………

II Neuroses………………………………………………………………………...........

III Other serious diseases……………………………………………………………….……

Date……………………………………………Signature…………………………

Station……………………………………... Designation………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OR– TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**

**SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-LUMYOZI**

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-LUMYOZI KIDATO CHA TANO Mchepuo wa …HGK/HKL…….. mwaka …2025/2026…. ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Dr.Samia-Lumyozi.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma Kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo changuliwa kusoma ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara. iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni. iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi

nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. ……………………………………………………… (Jina la mzazi) Kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi …………………………………… Tarehe ……………………………………………

---

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ………………………………………………………………………… ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………………………. Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari DR.SAMIA-LUMYOZI mwaka 2025. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.

Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………………..

…………………………………………………………………….
Simu ………………………………………………………….. Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi ……………………………………….Tarehe ………………………….

**‘’TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

## F. VITABU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na baadhi ya vitabu kutokana na masomo (Mchepuo) anayokuja kusoma hapa shuleni. Mwanafunzi atakaguliwa vitabu hivi mara tu atakapofika shuleni.(NB Unaweza kuvipata Duka la shule)

1. **ACADEMIC COMMUNICATION**

   Kila mwanafunzi **lazima** aje na kitabu cha somo la Academic Communication By TIE

2. **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

   Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kitabu cha somo la Historia ya Tanzania na Maadili kidato cha tano Kilichoandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania.

3. **ENGLISH**

**Jedwali Na. 1:** Orodha ya Vitabu Vilivyoteuliwa kwa Ajili ya **English Language** Ngazi Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita

| Na. | Jina la Kitabu | ISBN | Namba ya Cheti | Mwaka wa Uchapishaji | Idadi ya Kurasa | Jina la Mwandishi | Jina la Mchapishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Novel (English) -Form Five and Six | | | | | | |
| 1. | Animal Farm | 978-9966-25-898-4 | 1899 | 2024 | 117 | George Orwell | East African Educational Publishers Ltd |
| 2. | Chasing the Leopard Finding the Lion | 978-9987-08-178-3 | 1909 | 2024 | 329 | Julie Wakeman-Linn | Mkuki na Nyota Publishers Ltd |
| 3. | The Opportunist Elite | 978-9987-763-01-6 | 1376 | 2023 | 227 | Nyambari C. M. Nyangwine | Mbesa Books Distributors |
| 4. | The Horizon Unveiled | 978-9987-483-19-8 | 1710 | 2011 | 237 | Fellowes Mwaisela | FGD Tanzania Ltd |
| | Play (English)-Form Five and Six | | | | | | |
| 1. | The Government Inspector | 978-9966-46-440-8 | 1897 | 2024 | 166 | Nikolai V. Gogol | East African Educational Publishers Ltd |
| 2. | An Enemy of the People | 978-9966-25-525-9 | 1907 | 2024 | 118 | Henrik Ibsen | East African Educational Publishers Ltd |
| 3. | A Taste of Heaven | 978-9976-102-57-4 | 1388 | 2023 | 44 | Farouk Topan | Mkuki na Nyota Publishers Ltd |
| | Poetry (English)-Form Five and Six | | | | | | |
| 1. | Summons: Poems From Tanzania | 978-9976-1-0295-6 | 1401 | 2023 | 138 | Richard S. Mabala et al. | Mkuki na Nyota Publishers |
| 2. | Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems | 978-9966-25-337-8 | 1906 | 2024 | 167 | Jared Angira | East African Educational Publishers Ltd |

| Na. | Jina la Kitabu | ISBN | Namba ya Cheti | Mwaka wa Uchapishaji | Idadi ya Kurasa | Jina la Mwandishi | Jina la Mchapishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Julius Caesar | 978-9966-25-870-0 | 1896 | 2024 | 153 | William Shakespeare | East African Educational Publishers Ltd |
| 4. | Man of Kafira | 978-9966-46-194-0 | 1902 | 2024 | 103 | Francis Imbuga | East African Educational Publishers Ltd |
| | | **Poetry (Literature in English)-Form Five and Six** | | | | | |
| 1. | Poets of Africa 7; Boundless Voices Poem From Kenya | 978-9966-46-380-7 | 1894 | 2024 | 248 | Arthur I. Luvai | East African Educational Publishers Ltd |
| 2. | The Bleeding Heart and Other Poems | 978-9987-483-10-5 | 1418 | 2009 | 135 | Shilia Kaaya | FGD Tanzania Ltd |

**Jedwali Na. 3:** Orodha ya Vitabu Vilivyoteuliwa kwa Ajili ya **Kiswahili** Ngazi ya Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita

| Na. | Jina la Kitabu | Namba ya Cheti | Mwaka wa Uchapishaji | Idadi ya Kurasa | Jina la Mwandishi | Jina la Mchapishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Riwaya (Kiswahili)- Kidato cha Tano na Sita** | | | |
| 1. | Dunia Uwanja wa Fujo | 1458 | 2023 | 250 | Euphrase Kezilahabi | Africa Proper Education Network |
| 2. | Ua la Faraja | 739 | 2007 | 406 | W.E. Mkufya | Mangrove Publishers |
| 3. | Mirathi ya Hatari | 1476 | 2023 | 96 | C. G. Mung'ong'o | Mkuki na Nyota Publishers Ltd |
| 4. | Wasifu wa Siti Binti Saad | 1479 | 2023 | 80 | Shaaban Robert | Mkuki na Nyota Publishers Ltd |

| Na. | Jina la Kitabu | Namba ya Cheti | Mwaka wa Uchapishaji | Idadi ya Kurasa | Jina la Mwandishi | Jina la Mchapishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Tamthiliya (Kiswahili)-Kidato cha Tano na Sita** | | | |
| 1. | Mukwava wa Uhehe | 1452 | 2023 | 187 | M. M. Mulokozi | Africa Proper Education Network |
| 2. | Shujaa Mirambo | 1449 | 2023 | 119 | Emmanuel Mbogo | Africa Proper Education Network |
| 3. | Usaliti Mjini | 1964 | 2024 | 103 | Francis Imbuga | East African Educational Publishers Ltd |
| | | | **Ushairi(Kiswahili)-Kidato cha Tano na Sita** | | | |
| 1. | Fumbo Linaloelea | 1486 | 2023 | 82 | Nyambari C. M. Nyangwine | Mbesa Books Distributors |
| 2. | Malenga wa Ziwa Kuu | 1960 | 2024 | 192 | Wallah Bin Wallah | East African Educational Publishers Ltd |
| 3. | Andamo, Msafiri Safarini | 1466 | 2023 | 114 | Mohammed Khelef Ghassani | Educational Books Publishers Ltd |
| 4. | Wosia wa Baba | 1943 | 2024 | 205 | Ahmed Mohamed Amanzy | Abantu Publications Ltd |

**E. VIFAA VYA USAFI**

Kila mwanafunzi ataleta kifaa kama ilivyoainishwa hapa chini Kila mwanafunzi lazima aje na vifaa vya usafi kama ifuatavyo

- Jembe moja lenye mpini
- Kwanja moja
- Ufagio laini wa kufagilia sakafu
- Fagio mmoja wa chelewa wenye mpini

**MFANO WA KITAMBAA SARE YA DARASANI**



**Kwa darasani**


**shamba dress (kushindia)**

**K**aribu sana shule sekondari Dr.samia-Lumyozi




**RAMADHANI SEIF MWEMA**
**MKUU WA SHULE**